
# WANAWAKE & ARDHI

HAKIARDHI

TOLEO LA 1 JANUARI 2018



## NAFASI YA SHERIA ZA ARDHI KATIKA KULINDA HAKI ZA WANAWAKE

## CHANGAMOTO YA USHIRIKI WA WANAWAKE KATIKA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI.

*Na CHACODE, Chalinze*

Wanawake wanaoishi maeneo ya vijijini wanakutana na masahibu mbalimbali kutokana na sheria na tamaduni za kijamii. Masahibu haya yanamnyima kabisa mwanamke nafasi ya kupata, kumiliki, kutumia ardhi kwa shughuli mbalimbali. Vilevile wanawake hawashirikishwi ipasavyo katika utatuzi wa migogoro ya ardhi ambayo kwa kiasi kikubwa inagusa maisha yao na familia.

Ingawa katika miaka ya karibuni mwamko wa wanawake katika kufahamu masuala ya ardhi umeongezeka hasa kutokana mafunzo yanayotolewa na serikali pamoja na wadau wengine yakiwepo mashirika yasiyo ya kiserikali. Kuongezeka mwamko wa wanawake katika masuala ya ardhi tafsiri yake ni kuwa wanawake hawa watakuwa mstari wa mbele kushiriki katika maamuzi

*Inaendelea uk. 4*

YALIYOMO

- CHANGAMOTO YA USHIRIKI WA WANAWAKE KATIKA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI. 1 & 4
- UMBALI KIKWAZO KWA WANAWAKE KATIKA KUTATUA MIGOGORO YA ARDHI VIJIJINI 3-4
- WANAWAKE WAHAMASIKA KUDAI HAKI YA KUMILIKI ARDHI NA MALI NYINGINEZO 5-6
- WANAWAKE WATAMBUA UMUHIMU WA KUANDIKA WOSIA 7-8
- HATIMAYE WANAWAKE SINGIDA WAANZA KUHOJI KUHUSU HAKI YA UMILIKI WA ARDHI 9
- HATIMAYE WANAWAKE SINGIDA WAANZA KUHOJI KUHUSU HAKI YA UMILIKI WA ARDHI 10-11

TAHARIRI

## UTANGULIZI



# WANAWAKE&ARDHI

*Nafasi Ya Sheria Za Ardhi Katika Kulinda Haki Za Wanawake*

Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sheria za Ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999 zinasisitiza juu ya haki sawa kwa mwanaume na mwanamke katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi kama sehemu ya mali ambayo kila raia wa Tanzania ana haki ya kumiliki kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na marekebisho yake.

Pamoja na kuwa Sera na Sheria za ardhi kutambua usawa katika umiliki wa ardhi bado tafiti zinaonesha kuwa wanawake hasa waliopo vijijini wanakumbana na unyanyasaji mkubwa kutokana na mila na desturi ambazo hazimpi nafasi kama anayopata mwanaume.

Kumekuwepo na kesi kadha wa kadha zikiwahusisha watoto wa kike waliokosa urithi wa ardhi kutoka kwa wazazi wao kwa sababu tu wao ni waolewaji kwahiyo ardhi ipo kwa waume zao. Halikadhalika tumeshuhudia kesi nyingine za wanawake wakinyanyaswa pindi waume zao wanapofariki hivyo kukosa haki ya kumiliki ardhi na nyumba walizochuma na waume zao wakati wa ndoa yao.

Kutokana na vitendo hivi kuendelea Shirika la Foundation for Civil Society linafadhili mradi wa kutetea haki za wanawake katika ardhi kwenye baadhi ya mikoa hapa nchini ikiwa ni pamoja na Pwani, Morogoro, Iringa, Singida, Manyara na Arusha. Mradi huu unatekelezwa na mashirika ya ngazi ya wilaya yaliyopo katika maeneo haya kwa kushirikiana na Taasisi ya HAKIARDHI.

Jarida hili linajumuisha matokeo ya utekelezaji wa mradi huu katika maeneo haya kwa lengo la kuhakikisha kuwa jamii na wadau wengine wanajifunza matokeo chanya pamoja na changamoto zinazowakabili wanawake. Kwa kusoma jarida hili utajifunza uzoefu kutoka maeneo mengine ambao ni muhimu sana katika kutetea haki za ardhi kwa wanawake.

**Heri ya mwaka mpya 2018.**

*Cathbert Tomitho*
***Mhariri***



# UMBALI KIKWAZO KWA WANAWAKE KATIKA KUTATUA MIGOGORO YA ARDHI VIJIJINI

*Na CHACODE, Chalinze*

Dhima mojawapo ya kuanzishwa kwa Mabaraza ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi ngazi ya Vijiji, Kata na Wilaya ilikuwa ni kusaidia Jamii husika katika kutatua migogoro inayowakabili katika maeneo husika na kujiepusha na gharama kubwa za nauli na malazi kufuata Mahakama maeneo ya mbali. Pamoja na utambuzi huu bado kuna changamoto kubwa ya umbali kwa wanavijiji na hasa wanawake kuyafikia Mabaraza ya Kata na yale ya Wilaya. Vilevile umbali na ubovu wa miundombinu ya barabara ni changamoto kwa wajumbe wa Mabaraza haya kwenda katika maeneo ya ardhi yenye migogoro.

Shirika la CHACODE katika utekelezaji wa majukumu yake ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya usimamizi na utatuzi wa migogoro katika Wilaya ya Chalinze lilibaini changamoto wanayokumbana nayo wanawake katika kuyafikia Mabaraza ya Utatuzi wa Migogoro ya ardhi. Kwa mfano, katika vijiji vilivyoko katika tarafa ya Talawanda, Pera na Msata ambapo kuna maeneo makubwa ya vijiji na wananchi wengi hukaa maeneo ya mbali ofisi za kijiji sehemu ambayo hutumika kusikiliza mashauri ya migogoro ya ardhi. Kama ilivyo ada shauri haliwezi kusikilizwa siku moja likaisha, kile kitendo cha kuja kusikiliza shauri mara kwa mara huchukua kiasi kikubwa cha nauli ambayo kwa wanawake wengi ni vigumu kuimudu. Wakati mwingine shauri linaahirishwa kusikilizwa upande mmoja (mlalamikaji au mlalamikiwa) kutokana na mmoja wao kutokufika. Mifano ifuatayo ya wanawake watatu, wawili wajane inadhihirisha hali halisi ilivyo.

**Mfano wa kwanza:** Mnamo Desemba 20, 2017 katika kijiji cha Mazizi kata ya Msata ni siku ambayo wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji hukutana kusikiliza mashauri mbalimbali ya ardhi. Lakini kwa siku hiyo hakukuwa na shauri jipya bali wajumbe walikuwa wakisikiliza moja kwa wiki mbili mfululizo kutokana na mlalamikiwa kutokuweza kufika shaurini kutokana na umbali.

**Mfano wa pili;** huu unamhusu mjane katika kijiji cha Malivundo ambaye aliolewa akiwa chini ya miaka kumi na minane, akapata watoto watano ingawa wote ni wa kike. Alipofiwa na mumewe mwaka 2011 alinyimwa haki ya kumiliki mali yoyote kwa sababu hakubahatika kupata mtoto wa kiume ingawa aliendelea kuishi hapo na mke mwenzake. Baadae aliamua kuhamia kijiji cha jirani cha Kisanga kutokana na matatizo ya muda mrefu ndani ya familia hiyo. Baada ya CHACODE kufanya uhamasishaji kwa kutumia mikutano ya hadhara alihamasika sana na akaanza kudai haki yake. Alianza kudai haki yake katika serikali ya kijiji cha Malivundo ambapo gharama ya usafiri wa pikipiki na anapoishi ni shilingi elfu kumi. Baada ya miezi kadhaa Mjane yule alishindwa kumudu gharama za usafiri na hivyo kupoteza haki yake.

**Mfano wa tatu;** unamuhusu mjane mwingine anayeishi katika kijiji cha Kisanga lakini anatumia na kumiliki shamba katika kijiji cha jirani cha Malivundo. Mjane huyu alipata taarifa kuwa shamba lake limevamiwa na kundi la watu. Huyu mjane alianza kwenda kwa mwenyeketi wa kijiji husika baada ya kupanga naye miadi hadi mara mbili aliamua kuwasilisha shauri lake kwenye baraza la ardhi. Mjane huyu alilalamika sana kwa maana alitumia nauli nyingi pasipo kupata nafasi kukutana na kiongozi pamoja na wale waliovamia shamba lake. Mjane huyu anadai ilimchukua muda mrefu kupeleka shauri lake kwenye baraza la ardhi kwa kuwa hakuwa na ada ya kuandikisha shauri kiasi cha shilingi elfu saba. Na pia wakati shauri likianza kusikilizwa atapaswa kuchangia kiasi cha fedha ili kuwawezesha wajumbe wa baraza kwenda kukagua eneo husika kabla ya kutoa maamuzi.

Mifano hii mitatu tofauti inabainisha kinagaubaga madhila yanayowakabili wanawake na wanajamii wengine katika utatuzi wa migogoro ya ardhi kwenye maeneo ya vijijini. Umbali kutoka wanapoishi wananchi na ofisi za Mabaraza haya ni mkubwa hivyo kugharimu fedha nyingi za usafiri na malazi. Vilevile umbali kufika katika mashamba yenye migogoro nayo ni changamoto kubwa inayowafanya hata wajumbe wa mabaraza haya kukacha kuhudhuria vikao vya maamuzi. Hitimisho, ni muhimu kwa viongozi wa Mabaraza ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kutoa kipaumbele katika usikilizwaji wa mashauri yanayowahusu wanawake ili kuwaepusha na kusafiri kwa muda mrefu na kwa gharama kubwa mara kwa mara. Wajumbe wa Mabaraza haya wakiacha kuchelewesha usikilizwaji wa mashauri haya kutatoa unafuu kwa wanawake kudai haki zao na kuhakikisha wanazilinda.

›› Inatoka uk. 1

yanayohusiana na usimamizi wa ardhi pamoja na utatuzi wa migogoro ya ardhi katika maeneo ya vijiji vyao. Pamoja na hivyo huwapa wanawake ujuzi wa vitendo kujua maana ya uongozi na changamoto za uongozi. Hayo yote kwa pamoja huwajengea wanawake wengi zaidi kupata ujasiri wa kufanya mambo makubwa kama ilivyo kwa wanaume.

Ili wanawake wengi zaidi washiriki katika usimamizi na utatuzi wa migogoro ya ardhi ni muhimu kuweka mifumo ambayo itavutia wanawake kushiriki mikutano na vikao vya kujadili masuala ya Maendeleo na usimamizi wa rasilimali. Kwakuwa pasipo kufanya hivyo wanawake wengi watakata tamaa kutokana na mifumo iliyopo sasa kumpendelea zaidi mwanaume. Ni muhimu kutambua kuwa mifumo inayojadiliwa hapa ni pamoja na sera, sheria, miundombinu na mitindo ya uongozi katika taasisi na kijamii. Hadi sasa mahali pengi maamuzi mengi hufanywa na wanaume. Ile dhana ya kusema wanawake hawawezi bado inaishi ndani ya mifumo hiyo iliyoanzishwa.

Mfano wakati wa utekelezaji wa mradi wa kuwajengea uwezo wa kiutendaji mabaraza ya ardhi ya kijiji na mabaraza ya usluhishi ya kata ilibainika kuwa ni wanawake wachache sana wanapewa nafasi ya kuongoza katika mabaraza hayo na wengi wao ni wajumbe tu wakawaida. Takwimu zinaonesha kuwa katika vitongoji kumi na kata tatu za mradi kuna wajumbe tisini ambao kati yao wanaume ni 55 na wanawake ni 35. Ili kupima kuhusu ushiriki wa mwanamke katika ngazi za maamuzi ikiwemo kushika nafasi za uongozi ulifanyika ulinganifu wa wadhifa na jinsia ambapo katika jumla ya wenyeviti kumi na tatu tisa ni wanaume na wanne ni wanawake dhana hiyo pia ilijirudia kwa nafasi ya katibu wa baraza kama inavyoonekana katika jedwali la 1. Takwimu hizi zinatoa picha kuwa bado nafasi ya wanawake kuongoza hata kwenye mabaraza ya ardhi ni finyu sana na nafasi za uongozi zinashikiliwa na wanaume.

**Jedwali la 1: Mchanganuo kwa kuzingatia jinsia nafasi za uongozi**

| | | Wadhifa | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Wenyeviti | Makatibu | Wajumbe | |
| Jinsia | Wanaume | 9 | 9 | 37 | 55 |
| | Wanawake | 4 | 4 | 27 | 35 |
| Jumla | | 13 | 13 | 64 | 90 |

*Chanzo: CHACODE, shughuli za mradi, 2017*

Hata wakati wa uundaji wa mabazara hayo idadi ya wanawake hulazimishwa kuwa watatu kwenye Baraza la Ardhi la Kijiji na wanne kwenye Baraza la Kata. Ingawa tafsiri ya Sheria inayounda Mabaraza ya Utatuzi wa Migogoro ya ardhi inataka wanawake wasipungue watatu au wanne na sio kwamba wasizidi idadi hiyo. Tafsiri hii ya sheria kwa yenyewe ni nzuri lakini kutokana usimamizi mbovu wa mifumo katika sehemu nyingi wakati wa kuunda mabaraza mfano ya kijiji ni ngumu kuona wanawake wanazidi watatu hii inawanyima fursa wanawake wenye uwezo wa kuongoza kwa maana zile nafasi zingine zinaonekana kuwa ni lazima zikaliwe na wanaume. Kwa hivyo ni vema tafsiri ya sheria kuzingatiwa ili wanawake waweze kushiriki ipasavyo katika utatuzi wa migogoro ya ardhi katika vijiji na kata.

Pamoja na hayo wanawake wachache wanaopata nafasi za kuongoza ni muhimu wafanye kazi kwa bidii ili kudhihirishia umma kuwa wana uwezo wa kutosha na wasibezwe. Mfano katika mabaraza ya ardhi mijadala ya hoja hutawaliwa na wanaume wanawake hukaa kimya kusikiliza tu na kutia saini maamuzi hii ni kukamilisha tu idadi ya washiriki.

Kwa kuhitimisha, ushiriki wa wanawake katika usimamizi na utatuzi wa migogoro ya ardhi hasa katika ardhi ya vijiji ni jambo la muhimu sana kutokana na ukweli kuwa wanawake ndio wazalishaji wakubwa katika ardhi. Wanawake ndio waathirika wakubwa wa migogoro ya ardhi hasa pale kunapotokea mapigano baina ya wakulima na wafugaji wanawake wao ndio huachiwa familia bila ya kuwa na uhakika wa chakula.



# WANAWAKE WAHAMASIKA KUDAI HAKI YA KUMILIKI ARDHI NA MALI NYINGINEZO

*Na ICISO, Iringa*



*Pichani juu ni Bi. Hamida Mohamed wakijiji cha Mahenge, akieleza namna alivyoweza kutumia mafunzo aliyopatiwa na ICISO kupata shamba kutoka kwenye familia yake ambayo hapo awali mashamba yote yaligawiwa kwa watoto wa kiume pekee.)*

Kabla Shirika la ICISO kuanza kutekeleza mradi wa elimu ya ardhi kwa wanawake katika Wilaya ya Kilolo, utafiti wa awali ulionyesha kuwa wanawake wengi hawakuwa wakirithi ardhi kutoka kwa wazazi wao kutokana na mila na desturi za makabila ya Wahehe na Wabena kutokuruhusu mtoto wa kike kurithi kwa wazazi wake.

Kwa mujibu wa mila na desturi hizi, watoto wa kike watakuta mashamba kwa waume zao pindi watakapoolewa. Ingawa tafiti na uzoefu unaonyesha kuwa sio kweli kuwa wanawake urithi ardhi kwa waume zao kwasababu pindi mume anapofariki mwanamke hufukuzwa kwa wakwe zake kwa sababu kuwa aliyemleta katika ukoo huo amekwishafariki dunia.

Baada ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika vijiji vya mradi wanawake wameanza kupata uelewa wa haki zao katika upatikanaji wa ardhi. Wanawake wengi wamefurahia kufahamu kuwa kuna njia kadhaa za upatikanaji wa ardhi ambazo ni pamoja na kununua, kugawiwa na serikali, kupewa zawadi na kurithi. Katika njia zote hizi mwanamke ana haki sawa na aliyonayo mwanaume katika kupata ardhi.

Katika vijiji kadhaa wanawake wamehamasika kudai haki ya kupewa ardhi kutoka kwa familia zao kwa kuwafafanualia Wazee wa koo kuwa nao pia wana haki sawa na watoto wa kiume katika urithi wa ardhi na mali nyinginezo na hawapaswi kubaguliwa au kunyanyaswa kwa namna yoyote ile. Katika mikutano mbalimbali inayofanyika ndani ya vijiji hivi na kuwakutanisha wanawake kumekuwepo na midahalo inayohamasisha wanawake kudai haki yao kwakuwa haki ya mwanamke mara nyingi ni haki ya watoto. Hamasa hii inakuwa kubwa kwasababu tayari kuna baadhi ya wanawake wamekwishafanikiwa kurithi ardhi kutoka kwa wazazi wao pasipo kusababisha migogoro yoyote hivyo kuwa chachu kwa wenzao.

Bi Hamida anaongeza kwa kusema kuwa;

*“Mimi kama mtoto wa kike familia yangu haikunipatia urithi wa mashamba kwa sababu tu nitaolewa kwahiyo mashamba yangu yapo kwa mume wangu. Lakini baada ya kupata mafunzo nilirudi kuomba ardhi katika familia ambapo nilikubaliwa na kupatiwa”.*



Pichani juu, Bi. Yunes Chang'a wa Kijiji cha Ukumbi, Kilolo akielezea namna alivyopewa mashamba na wazazi wake baada ya kupata elimu ya Sheria za Ardhi. Bi. Yunes anasema yeye alikata tamaa ya kumiliki ardji yake mwenyewe kutokana na kukosa urithi vilevile kutokuwa na pesa ya kununua ardhi. Ila baada ya mafunzo alipata ufahamu wa kutosha kuhusu haki ya mwanamke na ardhi. Hivyo aliamua kurudi nyumbani na kuwaelemisha wazazi na ndugu zake wa kiume ambao walimuelewa na kumpatia ardhi kama urithi wake. Bi Yunes, aliwashauri wanawake wenzake kutokata tamaa pale wanapoomba haki ya kupewa mashamba kwakuwa bado Wazee wengi wana imani na mila zinazowakandamiza wanawake. Vilevile aliwasihi wanawake wenziwe kukaa na waume zao na kujadili juu ya mustakabali wa mali walizozichuma wakiwa pamoja ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima hapo baadae.

> *"Mimi nimeitumia elimu niliyoipata kuomba mashamba kwa familia yangu na wamenipa hivyo basi nawaomba wanawake wenzangu tusikae na faida hii peke yetu tuwasaidie wenzetu pia wapate mashamba"*
>
> alieleza Bi. Yunes

Hitimisho, ni muhimu sana wanawake wenyewe kuwa chachu ya kuwahamasisha wanawake wenzao katika kudai haki za ardhi katika vijiji vyao. Kwakuwa kwa kufanya hivyo wanawake ambao bado wako nyuma kiuelewa watajenga imani haraka na kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa ardhi inatunzwa na kulindwa kwa maslahi ya familia na jamii nzima.

# Wanawake watambua umuhimu wa kuandika wosia

*Na ICISO, Iringa*



Eneo jingine ambalo wanawake wa Wilaya ya Kilolo wamekuwa na uelewa nalo toka mradi huu wa haki za ardhi kwa wanawake unaotekelezwa na Shirika la ICISO kwa ufadhili wa Shirika la Foundation for Civil Society ni uandishi wa wosia. Katika uandishi wa wosia wanawake wengi wamebaini ukweli na umuhimu wa wazazi kuandika wosia ili kulinda mali za familia zisinyakuliwe na ndugu au watu wengine pindi mzazi au wazazi wanapofariki.

Hapo awali kabla ya mafunzo ilionekana kuwa kuandika wosia ilikuwa ni sawa na kujichuria kifo kwahiyo hakuna mzazi ambaye alikubali kuandika wosia kwa kuogopa kifo. Ingawa kulikuwa na mifano mingi sana ya watoto ambao walinyanyasika baada ya wazazi wao kufariki pasipo kuandika wosia na kuacha ugomvi mkubwa baina ya ndugu katika mali.

Baada ya mafunzo baadhi ya wanawake walionyesha mwamko wa wao wenyewe kujifunza namna rahisi ya kuandika wosia kwa mujibu wa sheria ili kulinda mali za familia ikiwa ni pamoja na ardhi. Kwa mfano Bi. Daines Makilika (pichani chini) wa kijiji cha Magana, kata ya Mahenge, Kilolo alisema kuwa;

*"Mimi kabla ya mafunzo haya sikutambua kwamba wosia ni muhimu sana na unaweza kuondoa migogoro isiyo ya lazima pale nitakapokuwa nimefariki. Kwa mfano, familia yangu watoto wangu wa kuwazaa wametawanyika sehemu mbalimbali kutafuta maisha. Kwa sasa naishi na watoto wa marehemu dada yangu ambao ni yatima na ndio wazalishaji wakubwa katika kilimo pale nyumbani. Baada ya elimu hii nimeona kuna umuhimu wa kuandika wosia utakaowajumuisha watoto wangu na wa dada katika mgawanyo wa mashamba ili kuepusha migogoro hapo baadae".*

Naye Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Mahenge Bi. Sheila Ngailo (pichani chini) alitoa ushuhuda wake mwenyewe wakati wa mafunzo kama ifuatavyo;

*"Nilidhulumiwa mali nilizotafuta na mume wangu wa ndoa halali ambazo ni nyumba na mashamba baada ya yeye kufariki. Ndugu wa mume wangu walinidhlumu mali hizo kwasababu nilikataa kurithiwa na shemeji yangu. Lakini laiti mume wangu angeandika wosia yote haya yasingetokea".*


Mh. Diwani anaongeza kwa kusema kuwa

*"Laiti kama mimi na mume wangu tungekua tumeipata elimu hii na wosia ukaandikwa nisingepata manyanyaso ya kunyang'anywa mali na ndugu wa mume wangu"*

Ni dhahiri kuwa elimu ya umuhimu na namna ya kuandika wosia imekuwa ya tija sana kwa wanawake na wananchi wote hasa kutokana na ukweli kuwa mila na desturi za makabila mengi nchini Tanzania hakuna utaratibu wa kuandika wosia kama njia rasmi ya kuhifahi mali katika mfumo rasmi wa kimaandishi.

Kwa kuhitimisha, ni jambo la kufurahisha kusikiliza na kusoma maelezo ya Bi Daines ambaye ameweza kuelewa umuhimu wa kuandika wosia ili kulinda ardhi na mali alizonazo zisivamiwe na watu wengine wakati wowote na kusababisha migogoro ya kifamilia. Bi. Daines anatoa somo kubwa na muhimu kwa wanawake wenzake na hata wanaume kuwa kuandika wosia sio kujitabiria kifo bali ni sehemu ya muhimu katika ulinzi wa mali za familia na kuiweka salama dhidi ya migogoro ya aina yoyote ile. Vilevile ushuhuda wa Mheshimwa Diwani unatoa angalizo kwa wazazi na watu wote ambao wanafikiri kuandika wosia ni suala la masihara.





# Elimu ya Sheria za Ardhi yaileta familia pamoja kumaliza mgogoro wa Ardhi uliowatenganisha kwa muda mrefu

*Na ICISO, Iringa*

Shirika la ICISO lilitoa mafunzo ya Sheria za Ardhi mnamo tarehe 26/08/2017 katika kijiji cha Chamgogo. Mafunzo haya yalihusu usimamizi wa ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi pamoja na masuala ya uandishi wa wosia. Baada ya mafunzo haya wananchi wengi walionyesha kuridhika na walichofundishwa hasa katika upatikanaji na umiliki wa ardhi na mali nyinginezo.

Mnamo tarehe 22/09/2017 familia ya marehemu mzee Paulo Kalinga ilimualika Mtendaji wa Kijiji cha Chamgogo Ndugu Innocent Kikoti na baadhi ya wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kusuluhisha mgogoro uliokuwa ukiikabili familia hiyo baada ya baba yao kufariki na watoto wa kiume kumiliki maeneo yote ya mashamba pasipo kumgawia dada yao.

Wanafamilia wa famila ya Marehemu Mzee Kalinga walisema katika kikao hicho kuwa baada ya mafunzo ya sheria za ardhi waliamua kukaa kikao cha pamoja kuona ni kwa jinsi gani wanaweza kumaliza mgogoro uliodumu toka mwaka 2014. Ujio wa mafunzo haya umeweza kutusaidia kwa kiasi kikubwa sana kutambua makosa yetu kwahiyo tumeamua kufanya usuluhishi wa mgogoro huu ili kila mwanafamilia apate haki yake kwa mujibu wa sheria.

Mgogoro huu ulishaletwa katika ofisi za Halmashauri ya Kijiji lakini ulishindikana kutatuliwa kutokana na wanafamilia hasa watoto wa kiume kutokufahamu Sheria za Ardhi zinasemaje juu ya haki za ardhi kwa wanawake. Mgogoro huu ulikuwa ni kero kubwa kwasababu dada wa familia hii alinyimwa haki ya kupata ardhi ya kulima kwajili ya kupata chakula kwajili ya familia yake.

Mgogoro huu ulifika sehemu ambapo ulizalisha makundi ndani ya ukoo wa familia hii na kupelekea ndugu kutokusalimiana na hata kutokushirikiana katika matukio ya kifamilia kutokana na chuki kubwa iliyojengeka baina ya wanandugu.

Katika kikao hiki cha usuluhishi mgogoro huu uliisha baada ya wana ndugu wa kiume kukubali kumpatia dada yao eneo la mashamba ili naye aweze kulima na kujipatia chakula kwajili yake na familia yake. Lakini usuluhishi huu usingewezekana pasipo elimu hii kupata kwanza na kuweza kuwafahamisha wananchi kufahamu haki za kila mwananchi katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi pasipo kujali jinsia ya mtu. Mafunzo haya pia yameweza kutoa mwongozo wa mamlaka na nafasi ya vyombo vya usimamizi wa ardhi ya kijiji kama vile Halmashauri ya Kijiji pamoja na kuainisha vyombo na mamlaka za utatuzi wa migogoro ya ardhi ambavyo ni Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji, Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Kwa kuhitimisha, ni muhimu kusisitiza ushiriki wa wananchi na hasa wanawake katika vikao na mikutano ya maamuzi yanayohusiana na rasilimali hasa hasa Mikutano Mkuu ya Vijiji, Vikao vya Halmashauri za Vijiji, Vikao vya Kamati ya Maendeleo ya Kata, Vikao vya Mabaraza ya Madiwani na vikao vingine kama hivyo lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanapata elimu zaidi ya usimamizi wa rasilimali, utatuzi wa migogoro na namna ya kunufaika na matumizi ya rasilimali hizo kwa jamii nzima.

# HATIMAYE WANAWAKE SINGIDA WAANZA KUHOJI KUHUSU HAKI YA UMILIKI WA ARDHI

*Na SIRVICONET, Singida*

Wanawake katika vijiji, mitaa na kata ambazo mradi wa haki sawa ya umiliki wa ardhi kwa wanawake unaotekelezwa na Shirika la SIRVICONET la mkoani Singida na kufadhiliwa na Foundation for Civil Society wameanza kuwa na mwamko wa kuhoji na kudai haki za ardhi. Taarifa hii inatokana na ripoti ya mtandao wa Shirika hili katika kipindi cha utekelezaji wa mradi ambapo wamepokea mashauri kumi na tano ya wanawake walioripoti kunyimwa haki zao juu ya masuala ya ardhi na kati ya hayo nane yameripotiwa katika sehemu husika na matano kupatiwa ufumbuzi ikiwa ni pamoja na kurudishiwa maeneo yao.

Mashauri mengine yanaendelea kufanyiwa kazi ingawa bado kuna wanawake wenye uoga wa kuripoti mashauri yanayowakabili kwa kuogopa kutengwa na jamii. Ongezeko hili la wanawake kuripoti migogoro ya ardhi inayowakabili ni kubwa ukilinganisha na mwaka 2016 ambapo hakukuwa na taarifa za kuonesha kuwa wanawake waliripoti vitendo vya kunyimwa haki zao za kumiliki ardhi.

Kutokana na mila na desturi za jamii ya watu wa Singida wanawake hawana haki ya kumiliki ardhi. Kutokana na kukosekana kwa mafunzo ya Sheria za Ardhi wanawake na jamii kwa ujumla walibaki na dhana ya kuwa wanawake hawana haki ya kumiliki ardhi isipokuwa wana haki ya matumizi ya ardhi kwa kulima mazao basi.

Hadi kutokana na mafunzo na mijadala inayoandaliwa na Shirika la SIRVICONET wanawake wameanza kujitokeza mstari wa mbele katika masuala ya ardhi kutokana na uelewa juu ya haki za msingi za wanawake zilizoainishwa katika Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 pamoja na sheria na sera nyinginezo zinazosimamia rasilimali nchini.

Kwa mfano, Bi. Juliana Njohome mwenye umri wa miaka 52 mkazi wa kijiji cha Mwankoko aliweza kuripoti na kuomba asaidiwe ili aweze kupata haki yake ya ardhi aliyochuma na marehemu mume wake aliyeishi naye kwa miaka kumi na tano [15]. Bi. Juliana alidhulumiwa mashamba baada ya shemeji zake [ndugu wa mume wake] kumfukuza kutokana nay eye kutokubarikiwa watoto katika ndoa yao. Kwa mila na desturi za jamii yake mwanamke anapokuwa hajababahatika kupata watoto katika ndoa basi pindi mumewe anapofariki mwanamke hupoteza haki zote za umiliki wa mali alizochuma na mume wake.

Mafunzo waliyopatiwa wanawake yameongeza ujasiri wao katika kudai haki za ardhi sio tu kwajili yao kama wanawake bali kwa familia nzima kutokana na ukweli kuwa wanawake wengi wanaishi katika ndoa ambazo wao ndio wazalishaji wakubwa wa chakula katika familia zao. Inatarajiwa kuwa wanawake wengi watajitokeza katika kudai haki za ardhi kadri utekelezaji wa mradi unavyoendelea.



*Pichani: Baadhi ya Wanawake mkoani Singida wakiwa katika mjadala wa masuala ya ardhi na wafanyakazi wa HAKIARDHI na SIRVICONET.*



# KONA YA SHERIA

## NAFASI YA SHERIA ZA ARDHI KATIKA KULINDA HAKI ZA WANAWAKE

> *Kwa upande wa rehani ya ardhi au nyumba katika ndoa, sheria imelinda maslahi ya wanandoa wote wawili.*

Katiba ya Tanzania inatoa haki ya kumiliki mali kwa kila raia. Haki hiyo pia inalindwa na Sheria ya Ardhi namba 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 za mwaka 1999. Kulingana na Sheria hizi, mtu au watu wanaoweza kuomba haki ya umiliki wa ardhi ni pamoja na mwanamke au mwanaume mtanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea. Hivyo wanawake wanaweza kupata ardhi kwa njia ya kununua, kupewa zawadi, kugawiwa na serikali au kugawiwa kurithi mila, desturi na taratibu za sheria husika. Wakati mila na desturi za makabila mengi nchini zinawanyima wanawake haki ya kupata, kutumia, kumiliki na ardhi.

Sheria za ardhi zimeondoa desturi za kibaguzi ambazo ziliathiri haki za wanawake kumiliki ardhi na kutambua usawa wa wanawake na wanaume katika kumiliki ardhi. Wanawake wana haki katika kumiliki ardhi kimila, haki ambayo hapo awali ilikuwa haipo na kama ilikuwepo basi ni katika baadhi ya mila na desturi nzuri japokuwa ni chache.

Wanawake wanapaswa watambue kuwa umiliki wa kisheria na wa kimila una hadhi sawa na wa mwanaume na pia kuna utaratibu wa kisheria mara baada ya kupata ardhi ili kuboresha umiliki wake ni hati maalum kulingana na eneo la ardhi au nyumba ilipo (mjini au kijijini).

Katika kulinda na kusimamia maslahi ya wanawake katika ardhi, Sheria za Ardhi za mwaka 1999 zimeainisha Mabaraza na Mahakama za utatuzi wa migogoro ya ardhi ambapo muundo wake umebainisha idadi ya wajumbe wanawake. Ukilinganisha na njia nyingine za kupata ardhi kama zilivyoainishwa hapo juu, utaratibu wa kupata ardhi kwa njia ya mirathi kwa mwanamke bado unasumbua hasa kwa makabila yanayoendeleza mila za kibaguzi. Hii ni kutokana na kukosekana kwa sheria moja ya mirathi ambayo inatumika kwa watu wote bila kujali dini, kabila wala rangi hivyo kusababisha wanawake kunyimwa haki ya kumiliki ardhi pindi waume zao wanapofariki.

Zipo aina tatu za nafasi ya mwanamke katika kumiliki ardhi kupitia mirathi. Moja, ni Sheria ya Mirathi iliyotungwa na Bunge inayotumika na Wakristo na watu wenye asili ya Ulaya. Pili ni Sheria ya Kiisalmu ihusuyo mirathi inayotumiwa na Waislamu. Sheria hizi mbili zinawapa wanawake (wajane) nafasi ya kurithi sehemu ya mali kwa mchanganuo maalum. Tatu ni Sheria ya Kimila inayosema kuwa mjane hawezi kurithi nyumba wala ardhi ya marehemu mume wake. Kama mjane atataka kuegemea katika sheria ya mirathi na kuachana na sheria ya kimila, anatakiwa kuthibitisha kuwa hajaishi katika ndoa husika kwa kufuata taratibu za kimila na kijadi ili aweze kurithi. Katika mahusiano ya ndoa, sheria za ardhi zinafafanua kuhusu umiliki wa ardhi kwa pamoja na usio wa pamoja.

Wanandoa wanaweza kuomba umiliki wa ardhi kwa pamoja katika maslahi yanayogawanyika au yasiyogawanyika. Katika umiliki wa pamoja kwa maslahi yasiyogawanyika inatolewa kwa wanandoa moja kwa moja na ndoa hiyo inapaswa iwe halali. Ila kwa watu ambao sio wanandoa, ni sharti kwanza wapate kibali cha Mahakama kupata umiliki wa aina hii katika ardhi husika. Katika umiliki wa aina yoyote yaani wa maslahi yanayogawanyika na yasiyogawanyika, ni lazima majina ya wamiliki wote yawepo kwenye hatimiliki na kila mmoja awe na nakala ya hatimiliki hiyo. Hivyo, nafasi ya mwanamke kwa maana ya maslahi yake katika umiliki wa aina hii ya ardhi inalindwa kwa kuwa hakuna mmiliki au wamiliki watakaoruhusiwa kuuza, kugawa, kuhamisha, kubadilisha umiliki au kuweka rehani ardhi pasipo kushirikisha mmiliki mwenzie na ridhaa yake kuainishwa kwa maandishi.

Sheria pia inaruhusu mwanandoa kumiliki ardhi binafsi. Katika hili ni sharti maslahi ya umiliki huu yawekwe bayana kuanzia awali pale mwanandoa mmoja wapo anapoomba umiliki wa ardhi husika. Mathalani, atapaswa kuainishwa kuwa anachukua hakimiliki hiyo kwa ajili yake binafsi kwa maslahi yasiyogawanyika. Kwa uzoefu wa misaada ya kisheria inayotolewa na Taasisi, jambo hili limeonekaana kusahaulika kwa wanandoa wengi katika jamii zetu.

Kisheria endapo umiliki huu binafsi ukiwa haujabainishwa tafsiri yake ni kuwepo na dhana ya kuwa wanandoa wote wanamiliki ardhi hiyo kwa maslahi yanayogawanyika, na Msajili wa hati atatakiwa kuwaandikisha wanandoa hao wamiliki kwa pamoja kwa maslahi yanayogawanyika. Wanawake wanapaswa kutambua nafasi hii kwani ardhi au nyumba wanazoishi katika ndoa mara nyingi ni wanaume wamenunua na kuweka majina yao peke yao, na kama haikubainishwa umiliki binafsi katika familia kwa maslahi yasiyogawanyika, ulinzi kisheria umewekwa kwa wanawake kunufaika na maslahi ya ardhi au nyumba husika kwa kuwa wengi wao huchangia nguvu kazi katika kuitunza au kuindeleza nyumba au ardhi na kuufanya ushiriki huu kumpa haki ya mgawanyo wa maslahi katika ardhi au nyumba husika

Kwa upande wa rehani ya ardhi au nyumba katika ndoa, sheria imelinda maslahi ya wanandoa wote wawili. Sheria inaelekeza pale ambapo ardhi au nyumba ya ndoa inawekwa rehani ni sharti ridhaa ya maandishi na sahihi ya mwanandoa halali wa mkopaji wanaoishi katika nyumba hiyo au kuitumia ardhi husika ipatikane na kinyume na hapo ni batili na pingamizi linaweza kufunguliwa mamlaka husika au mahakamani. Pia sheria imeainisha zaidi ni wajibu wa mkopeshaji kabla ya kutoa mkopo kuchukua hatua za makusudi za kuthibitisha kwamba mkopaji ana ndoa na kwamba anayetoa ridhaa ni mwanandoa halali wa mkopaji. Vilevile, iwapo mwanandoa atataka kuuza, kukodisha, au kuhamisha maslahi ya hakimiliki ya ardhi au nyumba ya ndoa kwa mtu mwingine, yule atakayehamishiwa, kuuziwa, kukodishwa au kupewa ana wajibu wa kuhakikisha kama ridhaa ya wanandoa wengine kama wapo imetolewa.

Pamoja na sheria hizi, bado kuna wanawake wengi hususan vijijini na maeneo ya pembezoni mwa miji wanaoshindwa kupata haki yao ya kumiliki ardhi kutokana na kukosa kuelewa sheria hizi au jinsi ya kudai haki zao kwa mujibu wa ulinzi uliowekwa kwao katika sheria za ardhi na nyinginezo. Mila na desturi kandamizi bado zipo hivyo elimu inahitajika zaidi ili watu waachane na mila hizo na kuhakikisha wanawake wanapata haki zao kama wanavyostahili.

HAKIARDHI
LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

TOLEO LA 1 | JANUARI 2018



Mradi huu unafadhiliwa na Foundation for Civil Society

THE FOUNDATION for Civil Society